



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI GEITA

Mtaa wa Bomanji, S.L.P 477, Geita. TANZANIA. Simu: 0282520296,
Nukushi 0282520159, Barua Pepe: info@geuwasa.go.tz, md@geuwasa.go.tz
Tovuti: www.geuwasa.go.tz



**YAH: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA KUBORESHA HUDUMA YA
MAJI MJI MDOGO WA KATORO-BUSERESERE**

SEPTEMBER, 2021

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu;

1. UTANGULIZI

Mradi wa maji wa Katoro-Buseresere ulianza mwezi Oktoba, 2020. Mradi ulikusudiwa kutekelezwa katika awamu tatu (3) kama ifuatavyo;

- i. AWAMU YA I : Ujenzi wa Tenki la maji lita 500,000
- ii. AWAMU YA II : Ujenzi wa Bomba kuu la Kusafirisha maji km 24.6 kutoka Chankorongo mpaka eneo la tenki jipya Katoro
- iii. AWAMU YA III : Ujenzi wa Bomba la kusambaza maji km 26, pamoja na ujenzi wa vituo vya kuchotear maji 10

Mji wa Katoro-Buseresere una wakazi wasiopungua **142,303** (2021) kutoka katika kata za Ludete, Nyamigota, Kaduda, Katoro na Buseresere. Mradi unaotekelawa kwa sasa unauwezo wa kuzalisha zaidi ya lita za ujazo 2,500,000 kwa siku na ukikamilika utahudumia wakazi wasiopungua **68,000**.

Aidha utekelezaji wa mradi huu ulipangwa kukamilika mwezi Juni 30, 2021 lakini mradi haukuweza kukamilika kwa wakati kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha, hivyo mradi umepangwa kukamilika mwezi Novemba 30, 2021. Mradi huu umelenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji katika kata za Katoro, Buserese, Nyamigota na Ludete. Mradi huu unatekelezwa kwa Force Account na Mamlaka ya majiSafi na Usafi wa Mazingira mjini Geita kwa gharama ya TZS. **TZS. 4,262,351,165.**

Mpaka sasa Kiasi cha **TZS. 2,184,952,318** sawa na asilimia **51.3%** kimetolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mamlaka imeingia mikataba mbalimbali ya watoa huduma/Wazabuni wa bomba yenyethamani ya **TZS. 2.81Bil** ambayo utekelezaji wake unaendelea. Mpaka sasa madeni ya Wazabuni ni kama ifuatavyo;

Jedwali Na.1: Madeni ya Wazabuni

Na	Mzabuni	Kazi	Kiasi katika Mkataba	Deni
1	KAHAMA OIL MILLS	Kuleta bomba na viungio km 32.5 kwa ajili ya kusafirisha maji na usambazaji.	1,516,567,529.60	1,516,567,529.60
	JUMLA		1,516,567,529.60	1,516,567,529.60

2. UTEKELEZAJI WA MRADI

Hadi kufikia mwezi Septemba 2020, Mamlaka ilikuwa imeshatekeleza mradi kwa **asilimia 70** na shughuli mbalimbali zilikuwa zimekamilika;

Jedwali Na.2: Utekelezaji wa Mradi

Na.	MAELEZO YA KAZI ZILIZOPANGWA KUFANYA	UTEKELEZAJI
1	Ulipaji wa fidia katika eneo la ujenzi wa tenki	100%
2	Ujenzi wa Nyumba ya mlinzi	90%
3	Ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita 500,000	100%
4	Ununuzi wa bomba na Viungio	100%
5	Ujenzi wa chemba katika tenki	0%
6	Ujenzi anchor block	70%
7	Ujenzi wa uzio wa tenki	80%
8	Kupasua mawe na Kusawazisha eneo la tenki	80%
9	Ukarabati wa bomba kuu linalofonya maji Ziwani(Ujenzi wa Sinker,usimikaji na alignment ya bomba)	100%
10	Ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji	0%
11	Ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji km 19.5 na bomba la kusambaza maji km 4.5	55%
12	Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji " Mobile treatment Plant"	0%
13	Ukarabati wa nyumba ya pampu eneo la Chankorongo	0%

3. UJENZI WA MOBILE TREATMENT PLANT KATIKA ENEO LA TENKI KATORO

Katika awamu ya IV, Mamlaka imepanga kuboresha utoaji wa huduma ya majisafi na salama, hivyo imepanga kujenga mobile treatment Plant katika eneo la tenki la Katoro ili kuyatibu maji hayo kabla ya kuwapatia wananchi.

4. MPANGO WA UKAMILISHAJI WA MRADI

Mamlaka imepanga kukamilisha awamu ya I,II na III mwishoni mwa mwezi Septemba,2021.

5. CHANGAMOTO ZILIZOPELEKEA MRADI KUTOKAMILIKA KWA WAKATI

Katika mpango wa utekelezaji wa mradi wa Katoro – Buseresere changamoto mbalimbali zimepelekea kuchelewa kwa ukamilishaji wake kama ifuatavyo;

- i. Uwepo wa mawe makubwa katika eneo la tenki na eneo linalopita bomba la kusambaza maji.
- ii. Mwamba mgumu baadhi ya maeneo
- iii. Kutopatikana kwa fedha za kutekeleza mradi kwa wakati

Imeandaliwa na



ENG. FRANK CHANGAWA

MKURUGENZI MTENDAJI

UTEKELEZAJI KATIKA PICHA

















